



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI



UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE JIMBO LA KWAHANI, ZANZIBAR TAREHE 08 JUNI, 2024

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Jimbo la Kwahani, Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar kuwa, kutakuwa na **Uchaguzi Mdogo wa Ubunge siku ya Jumamosi tarehe 08 Juni, 2024**. Hii ni kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 49(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

1. **SIKU:** Wananchi watapiga kura siku ya Jumamosi tarehe 08 Juni, 2024
2. **VITUO:** Zoezi la kupiga kura litafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 1:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 10:00 kamili Jioni

Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi

1. Mpiga Kura anatakiwa kwenda katika kituo alichojiandikisha na kadi yake ya mpiga kura siku ya uchaguzi.
2. Wapiga Kura, watakoruhusiwa kupiga kura ni wale walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).
3. Mpiga Kura akifika kituoni anatakiwa kupanga mstari, kutakuwa na mstari wa wanawake na wanaume.
4. Mpiga kura anatakiwa kufuata maelekezo yote atakayopewa na Karani Mwongozaji wa kituo.
5. Mpiga kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwa wapiga kura wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni.
6. Watu wenye mahitaji maalum wanaruhusiwa kwenda kituoni na wasaidizi.
7. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili Jioni kama wapiga kura bado wapo kwenye mstari, mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la-kupiga kura litaendelea hadi wapiga kura walio kwenye mstari watakapomalizika. Mpiga kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupiga kura.
8. Baada ya kumaliza kupiga kura, mpiga kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupiga kura.

Kumbuka kupiga kura ni haki yako ya msingi jitokeze siku ya uchaguzi Jumamosi tarehe 08 Juni, 2024 ukamchague Mbunge unayemtaka siku ya Jumamosi tarehe 08 Juni, 2024

Limetolewa leo tarehe 22 Mei, 2024 na:

Kailima, R. K.
MKURUGENZI WA UCHAGUZI